# Je niutaratibu gani wa kubadilisha kazi nchini Qatar?

State of Qatar
وزارة العمل
MINISTRY OF LABOUR

Wafanyakazi wote katika Jimbo la Qatar wanawe za kubadilisha kazi pasipo Cheti cha Hakuna Pingamizi (NOC).

*Hatua zilizopo hapa chinizinatumika kwa wafanyakazi wa sekta binafsi ambao Sheria ya Kazi Namba 14 ya 2004 inawahusu, wafanyakaziwandani, wafanyakazi wa kilimo na malisho ya mifugo, na wavuvi. Ili kubadilisha waajiri, hatua zifuatazo zinapaswa kufuatwa:*

### 1 Mfanyakazi anapaswa kutuma ombi la kubadilisha kazi kupitia mfumo wa kielektroniki wa Wizara ya Kazi (MoL):

- Mfanyakazi lazima achapishe, ajaze na kutia saini fomu ya"**Badilisha Mwajiri**". Mwajiri mpya pia anahitaji kutia saini na kugonga muhuri rasmi wa kampuni kwenye fomu. Ikiwa mfanyakazi anabadilisha kazi kufanyaka-zi katika nyumba ya mtu binafsi, saini ya mwajiri mpya itatosha.
- Mfanyakazi lazima aingie kwenye **mfumo wa kielektroniki wa MoL** na kitambulisho chake cha (QID) na nambari ya simu ya mkononi, na kasha kupakia nakala ya fomu iliyotiwa saini. Nambari ya simu ya mkononi lazima iunganishwe na QID ya mfanyakazi.

### 2 Mara tu ombi linapokuwa limetumiwa, nambari ya EC (Badilisha Mwajiri) itaonekana kwenye skrini. Nambari hii inathibitisha kwamba ombi limewasilishwa kwa ufanisi.

- Wafanyakazi wanapaswa kuweka kumbukumbu ya nambari ya EC.
- Wakati wowote wafanyakazi wanaweza kuangalia hali ya ombi lao kwa kuingia kwenye **tovutiya Wizara** kwa kutumia nambari zao za QID na EC.
- Wafanyakazi wanaweza kughairi ombi lao wakati wowote kabla ya ombi kuidhinishwa, kupitia **mfumo wa kielektroniki wa MoL**
- Wafanyakazi wanaweza kughairi ombi lao baada ya kupokea kibali kwa kutuma ombi lililoandi kwa kwa MoL, ilimradi tu mkataba wao mpya wa ajira haujaidhinishwa bado. Wanapaswa kutuma barua iliyotiwa saini kwa Kiarabu iliyotumwa kwa Mkuu wa Idara ya Mahusiano ya Kazi. Katika barua hii, wanapaswa kujumuisha maelezo mafupi kwa nini wanaomba kughairi ombi lao pamoja na nambari ya EC iliyotolewa wakati wa kutuma ombi, nakala ya QID yao na nambari ya simu ya mkononi.

### 3 Wizara inaweza kukataa ombi la kubadilisha kazi iwapo, kwa mfano, mfanyakazi hakujaza fomu kwa usahihi au mwajiri mpya anazuiwa kuajiri wafanyakazi wapya.

### 4 Mara tu ombili linapokuwa limeshughulikiwa, mfanyakazi atapokea ujumbe mfupi wa simu kutoka Wizarani ukithibitisha mabadiliko ya ajira na kipindi cha notisi.

Ni katika hatua hii ambapo waajiri wa sasa na wapya watajulishwa.

- Ikiwamfanyakazi amefanya kazi kwa mwajiri wa sasa kwa miaka 2 au kwa muda usiozidi huo, kipindi cha notisi kitakuwa mwezi 1.
- Ikiwa mfanyakazi amefanya kazi kwa zaidi ya miaka 2, kipindi cha notisi kitakuwa miezi 2.
- Mwisho wa kipindi cha notisi utaonyeshwa kwenye ujumbe mfupi wa simu kutoka Wizarani.
- Mfanyakazi lazima aendelee kufanya kazi na mwajiri wa sasa katika kipindi cha notisi isipokuwa kama mfanyakazi na mwajiri wa sasa wamekubaliana kupunguza kipindi cha notisi.

### 5 Mara tu kipindi cha notisi kinapokamilika, mwajiri mpya atatayarisha mkataba wa ajira kupitia Mfumo wa Uthibitisho wa Kidigitali wa MoL kwa Mkataba wa Ajira wa Lugha Nyingi.

Hili inahitaji kukamilika ndani ya miezi mitatu kutoka mwisho wa kipindi cha notisi cha mfanyakazi. Baada ya kujaza taarifa zote, mwajiri mpya atachapisha mkataba wa ajira utakaotiwa saini na mfanyakazi na mwajiri mpya. Ikiwa mfanyakazi anakubaliana na masharti katika mkataba, anaweza kutia saini.

- Mwajiri mpya atapakia mkataba uliotiwa saini kwenye tovuti ya Wizara kwa ajili ya uthibitisho.
- Baadaya kukamilika, mwajiri mpya lazima atoe nakala ya mkataba wa ajira uliothibitishwa kwa mfanyakazi.

### 6 Baada ya mkataba wa ajira kuthibitishwa, mwajiri mpya anapaswa kutuma ombi la QID mpya ya mfanyakazi kwenye Wizara ya Mambo yaNdani.

### 7 Mfanyakazi sasa anaweza kuanza kazi yake hiyo mpya

Mfanyakazi atapokea QID mpya (bila malipo) kutoka kwa mwajiri mpya.

## *Kumbuka*

Wafanyakazi na waajiri wanaweza kupakua nakala ya mkataba wa ajira wakati wote kupitia **tovutiya MoL**.

## *Viunganishi muhimu*

**Tuma ombi lako la kubadilisha kazi**

**Angalia hali ya ombi la kubadilisha mwajiri wako**

**Tuma lalamiko linalohusiana na kazi kwa MoL**

## NITAPATA WAPI TAARIFA ZAIDI?

Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na Wizara ya Kazi kwa simu ya moja kwa moja **40288101**, Barua pepe **info@mol.gov.qa**, Tovuti **www.mol.gov.qa** au tembelea ofisi zetu.